

Mtanzania

Penye nia pana njia

ISSN 0856-5678

TOLEO NA. 3022

Jumane, Agosti 10, 2004

TANZANIA

B

Kikundi cha dini kujenga kituo cha vijana

**na nathan mtega, pst,
songea**

KIKUNDI cha vijana wa Marekani kijulikanacho kama Miracle Corner of the World, kinatarajia kuanza ujenzi wa kituo cha kisasa cha maendeleo ya vijana katika kata ya Ruvuma, wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Kituo hicho cha kisasa kinajengwa kwa ajili ya shughuli mbali mbali za uchumi kwa vijana na burudani mbali mbali.

Kiongozi wa kikundi hicho, Edward Bargman, alisema kuwa kituo hicho kinalenga kuwakomboa vijana wa wilaya hiyo

kiuchumi na kielimu.

Alisema ya kuwa kituo hicho kitatoa mafunzo ya ufundi wa aina mbali mbali, ukiwamo ujenzi, useremala na mengine kwa lengo la kupunguza kasi kubwa ya vijana kuzurura kwa kukosa shughuli za kufanya.

Bargman alisema ya kuwa majengo 40 yatajengwa kwa ajili ya kuanzia na baadaye yataongezwa mengine kulingana na mahitaji.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Songea, Abed Mwinyimisa, aliwaomba wananchi wa kata hiyo ya Ruvuma na wilaya kwa ujumla kutoa ushirikiano wa karibu wa vijana wenye nia ya kuleta maendeleo wilayani humu.